



Hatua za kupata Leseni Yako ya Kuendeshea gari

Ni kinyume cha sheria kuendesha gari nchini Australia Magharibi bila leseni au kibali cha kuendeshea gari kilichoidhinishwa. Ukiukaji wa sheria hizi kunaweza kusababisha:- kushtakiwa na Polisi wa WA, kushtakiwa Kortini, faini, kifungo, na kushtakiwa na watu walioumia.

Hizi ni hatua 6 za kupata leseni yako ya kuendeshea gari ya Australia Magharibi.

HATUA YA 1
KIBALI CHA WANAFUNZI

- Lazima ufanye mtihani wa nadharia wa kunena na wa kompyuta juu ya sheria za barabara.
- Lazima ubebe Cheti chako cha Kuzaliwa, pasipoti, visa au cheti cha uraia ili kujitambua.
- Lazima pia ubebe kadi ya huduma ya Afya, kadi ya huduma ya Matibabu au kadi ya benki na hati ili zionyeshe saine na anwani yako ya sasa.
- Itakubidi ulipe kiasi cha pesa. Pesa hizo ni za mtihani wa nadharia na kibali cha wanafunzi kama utapita mtihani. Zinalipia pia mtihani wako wa uendeshaji gari.

HATUA YA 2
KUJIFUNZA KUE-
NDESHA GARI

- Unaweza kuanza kujifunza kuendesha gari na mtu ambaye amekuwa na leseni ya aina hiyo moja kwa miaka isiopungua 4.
- Lazima ubebe kibali cha mwanafunzi unapokuwa ukiendesha gari.
- Daima lazima uwe na pleti za L kwenye gari lako unapokuwa ukijifunza kuendesha gari.
- Hakuna pombe unapokuwa ukiendesha gari.

HATUA YA 3
MTIHANI WA UENDESHAJI GARI

- Lazima uwe angalau na umri wa miaka 16 na miezi 6.
- Lazima uwe na gari nzuri unapokuwa ukifanya mtihani. Mtihani wako wa kwanza wa uendeshaji gari umelipiwa unapopata kibali cha mwanafunzi. Ukianguka kwa mara ya kwanza, itakubidi ulipe pesa zaidi kwa kila mtihani.

HATUA YA 4
BATLI

- Ukipita mtihani wako wa uendeshaji gari utapewa batli.
- Lazima ulipe kiasi cha pesa kwa ajili ya batli.
- Lazima ukamilishe angalau masaa 25 ya uendeshaji gari kwa kusimamiwa.
- Lazima urekodi kila somo katika batli hii.
- Ni hati halali kwa hivyo kila kitu kinachorekodiwa ndani lazima kiwe cha kweli, kiwekwe saine na kuwe na mshahidi.
- Daima lazima uwe na pleti za L kwenye gari lako unapoendesha gari.
- Hakuna pombe unapokuwa ukiendesha gari.

HATUA YA 5
MTIHANI WA HATARI

- Kabla upate leseni yako itakubidi upite mtihani kwa kompyuta ili uone kama unaweza kupambana na hali tofauti za trafiki na ufanye maamuzi salama ya uendeshaji gari.
- Lazima uwe na umri wa miaka 17.
- Batli lazima ikamilishwe ikiwa na masaa 25 yaliyonakiliwa ya uendeshaji gari kwa kusimamiwa na kuwekwa saine na wewe na mkufunzi au msimamizi wako wa uendeshaji gari.
- Beba batli na kitambulisho kwa kituo cha kutoa leseni au ajenti wa kutoa leseni.
- Itakubidi ulipe kiasi cha pesa ili ufanye mtihani.

HATUA YA 6
LESENI

- Ukikamilisha hatua zote hapo juu na upite mitihani yote utapata leseni yako.
- Utapigwa picha ya leseni yako.
- Itakubidi ulipe kiasi cha pesa ili upate leseni yako.
- Hakuna pombe unapokuwa ukiendesha gari.



Department for
Planning and Infrastructure
Government of Western Australia

DRIVE SAFE. ARRIVE SAFE.



www.officeofroadsafety.wa.gov.au